AYANA INTERNATIONAL

MAABALA YA UBUNIFU KWA VIJANA

MWONGOZO KWA WAWEZESHAJI

Kujihusisha & kuwezesha kizazi kinachofuata cha viongozi ili kubadilisha jamii zao na kuwa bora zaidi.

WWW.AYANAINTERNATIONAL.ORG

WAKATI VIONGOZI WAKIJIANDAA KUCHUKUA MITAZAMO MIPYA YA KULETA MAENDELEO YA KUDUMU, USHIRIKA WA VIJANA NI WA THAMANI SANA KIPINDI HIKI KULIKO MUDA WOWOTE ULE. KATIKA MUDA HUU WA KIHISTORIA NINAWAHIMIZA VIJANA KUDAI NA KUTUNZA MAENDELEO YA KASI YANAYOHITAJIKA SANA DUNIANI KWETI.

BAN KI MOON
ALIYEKUWA KATIBU MKUU UN

KUHUSU AYANA

AYANA ni shirika la kimataifa 501(c)(3) lisilo la kibiashara lililosajiriwa na lenye malengo ya kuvuna nguvu kazi ya raslimali muhimu kabisa jamii yoyote ile: ambayo ni vijana. AYANA inafanya kazi kwa kushirikiana na NGO na CBO ambazo ni washirika wake katika nchi zinazoendelea ili kuweza kutekeleza Maabala za Kibunifu kwa Vijana (Youth Innovation Labs), warsha za wiki nzima zilizoandaliwa ili kuwawezesha vijana kutengeneza suluhisho kwa mambo yatakayonufaisha jamii zao wenyewe. Kupitia hatua ya kipekee ambayo inahusisha uongozi na maendeleo, kutafakari kwa kina, utatuzi wa matatizo kwa ubunifu, kushirikiana, upangaji wa mikakati, na zaidi, Maabala ya Ubunifu kwa Vijana inawapatia washiriki wake na ujuzi wa kuwa viongozi wa sasa huku ikitoa mwangaza kwa miaka ya mbeleni. Misheni yetu ni kuwawezesha vijana kwa kuwapatia ujuzi utakaowawezesha kubadili jamii zao zinazowazunguka, na kuruhusu matatizo makubwa yanayozikabiri nchi zinazoendelea kuweza kupatiwa na ufumbuzi wa muda mrefu na wa kudumu. Maono yetu ya mbali ni kuona dunia ambayo kila kijana anauelewa juu ya uwezo wake wa kusababisha mabadiliko na anapewa nafasi ya kuweza kutekeleza uwezo wake huu.

MAARIFA YA MUHIMU YA KUKUZWA



Kwa muda wa programu yetu, vijana watakuza maeneo muhimu 6 kama viongozi. Kwanza ni uwezo wa kupanga na kuongoza wengine ndani ya jamii zao. Pili ni uwezo wa kufikiria kwa kina juu ya changamoto zinazokabili jamii zao na kuchunguza mizizi ya matatizo yanayosababisha. Tatu ni kutatua matatizo kwa kutumia ubunifu na kuwa na hisia katika kugundua suluhu. Nne ni uwezo wa kushirikiana na watu wengine wanaotoka katika mazingira tofauti tofauti na wenye uwezo mbalimbali katika timu. Tano ni uwezo wa kuwasilisha mawazo yao kwa ufasaha, ambao wanaukuza kwa kupitia utoaji wa hotuba wa mara kwa mara katika kipindi chote cha warsha. Na ujuzi wa mwisho ambao washiriki wataukuza ni uwezo wa kupanga kwa umakini ikiwemo kuweka malengo na kuyatimiza. Maeneo ambayo tumejikita yanatokana zaidi na mifumo iliyotokana na utafiti yenye kuwa na maarifa yanayohitajika zaidi ili kuweza kufanikiwa katika karne ya 21, ikiwemo ‘4Cs’ na ‘Formative Five’.

KUAMSHA UWEZO WA KUWA KIONGOZI

Muda: Dakika 30-45

Waulize wanafunzi wataje viongozi ndani ya familia zao, shule, jamii, nchi au duniani kiujumla. Kisha, kujadili kama kundi:

- Ni sifa zipi za uongozi kiongozi wako anazo?
- Ni sifa zipi za uongozi alizonazo kiongozi wako na wewe pia unazo?
- Ni maarifa gani ya uongozi ambayo kiongozi wako alijifunza katika maisha yake?
- Ni mambo/mifano gani ambayo yanaonyesha uongozi katika maisha ya kiongozi wako?

Inamaanisha nini kuwa kiongozi?

Kutokana na wazo la uongozi wa mabadiliko, kiongozi bora ni mtu ambaye anatengeneza maono ya kutia moyo kwa nyakati zinazokuja na kuwahamasisha pamoja na kuwapa moyo watu ili kuweza kushirikiana nae katika maono yake hayo.

Kugundua Uwezo wa Uongozi

Sasa wanafunzi watajaribu kugundua uwezo uliopo ndani yao wa uongozi huku wakijiandaa kutengeneza timu za kushirikiana. Gawanya kadi kwa kila mwanafunzi. Kwenye upande mmoja waambie waandike mambo matatu(3) makubwa ambayo ni uwezo walionao (kama umakini, mpangiliaji, mwenye mantiki, mbunifu) na kwenye upande mwingine waambie waandike madhaifu yao makubwa matatu(3) (kama vile upangiliaji, kwenda na muda, kuwasiliana). Wape wanafunzi dakika 5 kuzunguka darasani na kutafuta wanafunzi wengine ambao wanauwezo unaoendana na madhaifu yao. Kisha, kwenye dakika 5 zinazofuata, waambie wanafunzi waseme udhaifu ambao wanao na jina la mtu ambaye walimpata ameandika kama moja ya uwezo wao.

MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU

Muda: Dakika 40-50

KUHUSU MCHAKATO HUU

Katika hatua hii, unatakiwa kuelewa eneo lako au maeneo yako husika katika Malengo ya Maendeleo Endelevu. Unatakiwa kusoma maelezo ya UN juu ya Malengo ya Maendeleo Endelevu na hatua ambazo jamii mbalimbali duniani zimepanga kuzichukua. Utatakiwa kugundua na kujifunza zaidi kuhusu matatizo yanayoathiri jamii yako moja kwa moja.

MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU

Malengo ya Maendeleo Endelevu ni sehemu ya ajenda pana ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2030. Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ni pamoja na kutokomeza umasikini, kutokuwa na njaa, afya bora na maisha stahiki, elimu bora, usawa wa kijinsia, maji salama na usafi, nishati mbadala kwa gharama nafuu, na zaidi.



“KUTOKOMEZA UMASIKINI NDIYO JAMBO LA MUHIMU KATIKA AJENDA YA MWAKA 2030, NA PIA PAMOJA NA AHADI YA KUTOMUACHA MTU YOYOTE NYUMA. AJENDA INATOA NAFASI YA KIPEKEE KUIWEKA DUNIA NZIMA KATIKA NJIA BORA YA MAENDELEO ENDELEVU.”

Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), yanayojulikana pia kama Malengo ya Dunia, ni malengo ya utekelezaji kidunia nzima ili kuweza kutokomeza umasikini, kulinda sayari na kuhakikisha watu wote wanafurahia amani na ustawi. Malengo yanakuwa yanaingiliana – mara zote ili moja lifanikiwe linakuwa likihusisha kufanikiwa kwa jambo lingine. Malengo haya yanafanya kazi kwa kutegemea ushirikiano na busara ili kuhakikisha vitendo sahihi vinafanyika kuboresha maisha, kwa namna ambayo ni endelevu, kwa vizazi vya mbeleni. Yanatoa muongozo ulio wazi na malengo ambayo nchi zote zinatakiwa kuyafuata kwa kufuata vipaumbele vyao wenyewe na changamoto za kimazingira kwa dunia nzima kiujumla. Malengo ya SDG ni ajenda shirikishi. Yanakabiriana na mizizi ya vyanzo vya umasikini na kutuunganisha kwa pamoja kuleta mabadiliko chanya kwa binadamu na sayari kwa ujumla. (UNDP)

Kitu cha Kufanya: Kutafuta Umakini
Kati ya malengo hayo hapo juu, ni malengo gani matatu ambayo unahisi yanakugusa wewe zaidi na maono yako katika jamii yako au mambo unayopendelea binafsi? Kwanini?

Majadiliano ya Kikundi
1. Ni malengo gani ya SDG yanakugusa zaidi wewe? Kwanini?
2. Ni kwanini malengo ya SDG ni ya muhimu?
3. Je, malengo ya SDG yanaweza kutimizwa?
4. Ni kwa namna gani tunaweza kutimiza malengo hayo?
5. Ni suala gani katika jamii yako inayokuzunguka umelichagua na kwanini?

UTAFITI WA MASUALA KATIKA JAMII

Muda: Dakika 30

Sasa umekwishapata Malengo ya Maendeleo Endelevu yanayokuvutia wewe, utaanza kuchunguza matatizo katika jamii yako ili kuanza kufikiria njia za kibunifu za kuyatatua.

Sambaza madaftari madogo kwa kila mwanafunzi. Kwa dakika 2, waambie watafakari na kuandika matatizo yote ambayo yana athari hasi kwenye jamii zao (mchakato huu unahitaji kuwa mwenye hisia, kama tulivyoongelea juu). Kisha, waambie waonyeshe jambo au mambo ambayo wanavutiwa zaidi kulitatua na kisha warudishe wanafunzi katika duara la majadiliano ya kikundi tena. Waulize wanafunzi waseme jambo 1 au mwisho 2 waliochagua.

Kisha, waambie watengeneze timu za kushirikiana ili kuweza kutatua tatizo hilo. Kama kuna mwanafunzi mmoja ambaye hana mwenzake kwa sababu jambo alilochagua ni jambo ambalo hakuna mtu mwingine alielichagua, muulize kama angependa kufanya kazi mwenyewe au kutafuta jambo lingine aliloandika ambalo watu wengine kwenye darasa wamelichagua pia, kashi ajiunge na timu hiyo. Kila timu inatakiwa kuwa na kama wanafunzi 3 mpaka 4.

Mjadala

1. Ni tatizo gani mmechagua?
2. Ni kwanini mmechagua tatizo hili?
3. Ni nani anayeathiriwa na tatizo hili?
4. Ni watu gani ambao ni wadau wakubwa?
5. Ni kwa muda gani tatizo hili limekuwepo?

KARATASI YA MAZOEZI YA MWANAFUNZI: RAMANI YA WADAU

Muda: Dakika 30

Sasa ukiwa umekwishagundua jambo katika timu yako, fanyeni kazi kutengeneza ramani yenye maelezo mafupi ya mdau/wadau wanaohusika. Jaribu kuwatambua kwa ufasaha kadri inavyowezekana.

Jina la Mdau: MIMI NILIPO _____ NILIHITAJI KU _____ ILI NIWEZE KU _____.
Jina la Mdau: MIMI NILIPO _____ NILIHITAJI KU _____ ILI NIWEZE KU _____.
Jina la Mdau: MIMI NILIPO _____ NILIHITAJI KU _____ ILI NIWEZE KU _____.
Jina la Mdau: MIMI NILIPO _____ NILIHITAJI KU _____ ILI NIWEZE KU _____.
Jina la Mdau: MIMI NILIPO _____ NILIHITAJI KU _____ ILI NIWEZE KU _____.

UPANGAJI YA SULUHISHO

MUDA: DAKIKA 50-60

Anza siku kwa kuvunja ukimya, sasa hivi zungumza zaidi katika kujenga timu.

Kufikiria Kimipango

Leo, tambulisha mchakato wa Kufikiria Kimipango. Tumia mchakato wa kufikiria kimipango wa karatasi ya mazoezi ya AYANA ili kuwapa wanafunzi utangulizi wa muhimu juu ya wazo hili. Fafanua kwamba kufikiria kimipango kimsingi inahusu kuwa na hisia na kutatua tatizo kwa ajili ya walengwa wako. Sambaza vikaratasi vidogo vya kubandika kwenye kila kundi na waambie washirikiane kupendekeza mambo ambayo yanaweza kuwa suluhisho kwa matatizo waliyoyagundua.

Mjadala

1. Kuna suluhisho gani linafanyika sasa hivi?
2. Ni kwa namna gani suluhisho lako lipo tofauti?
3. Ni kwa namna gani wazo lako linatumia hisia katika kutoa suluhisho bora?

Kofia Sita za Kufikiria

Sambaza karatasi za mazoezi za Kofia Sita za Kufikiria. Mbinu hizi za kufikiria zitawaruhusu kuchunguza kila suluhisho lililopendekezwa kwa mtazamo mpana zaidi, kwa kuzingatia pande zote (mambo bayana, mambo hasi, mambo chanya, n.k.) Kofia sita za kufikiria ni: Mchakato (kupanga na kuweka mipango), mambo bayana (yasiyo upange wowote na mambo halisi), hisia (uelewa na hisia), ubunifu (suluhisho, mawazo), faida (zilizo chanya), na athari (ni nini kinaweza kwenda vibaya?). Waambie wapitie mambo yote haya.

KARATASI YA MWANAFUNZI YA MAZOEZI: UPANGAJI WA SULUHISHO

MUDA: DAKIKA 45

Kuchangia mawazo: Ni kwa namna gani unaweza kutatua tatizo hilo?=

Jifunze: Ni taarifa gani bado tunazihitaji?

Tengeneza: Tengeneza suluhisho lako mwenyewe la tatizo hilo.

Tathmini: Ni kwa namna gani unaweza kupima mafanikio?

Rekebisha: Ni madabiliko gani tunahitajika kuyafanya?

Shirikisha: Ni kwa namna gani tunaweza kushirikisha suluhisho hili na watu wengine?

KARATASI YA MAZOEZI YA MWANAFUNZI: KOFIA SITA ZA KUFIKIRIA

MUDA: DAKIKA 30

VITU CHANYA, FAIDA, MAENDELEO, FAIDA, MATARAJIO MEMA

Ni maeneo gani ni mazuri? Ni kwanini unapendelea hapa? Ni kwa namna gani tunaweza kufanya hii ikafanya kazi?

POINTI DHAIFU, MAMBO HASI, UBAYA WAKE, MAENEO MABAYA, UKOSEFU WA MATUMAINI

Hii ina tatizo gani? Ni nini tunapaswa kuwa makini nacho? Ni nini kinapaswa kuboreshwa?

KUCHUNGUZA, KUPANGA, KUTAFAKARI, KUFIKIRIA

Ni fikra gani bado zinahitajika? Tunaweza kupangaje jambo hili? Hatua yetu itakayofuata itakuwa ipi? Muhtasari wa haya ni ukoje?

MAPENDEKEZO, UWEZEKANO, SULUHISHO, NJIA MBADALA

Mapendekezo yetu ni yapi? Je, kuna mawazo mengine? Je, kuna njia zingine mbadala? Je, kuna namna nyingine ambavyo tunaweza kulifanya hili jambo?

NAMBA, TAARIFA, MAELEZO, USHAHIDI

Je, tuna taarifa zipi? Je, tunahitaji taarifa gani? Je, taarifa gani zinakosekana? Je, tutazipataje taarifa hizo?

HISIA TUNAZOPATA, HISIA TUNAZOHISI, MAKISIO, MAKADIRIO

Ni nini tunachokihisi juu ya jambo hili? Ni kwa namna gani tunaweza kusisitizia? Ni yapi makisio yako?

USIMAMIZI WA MRADI

MUDA: DAKIKA 30-40

Wanafunzi wataanza kuweka mipango mkakati na mchakato wa kuweka bajeti kwa ajili ya miradi yao. Hii ni jambo la muhimu sana kwa mradi kuwa wa mafanikio na wenye matokeo.

Mipango Mkakati

Fungua 'Powerpoint' ya AYANA sehemu ya Usimamizi wa Mradi ili kuwapatia wanafunzi utangulizi juu ya mipango mkakati, ushirikiano, na upangaji wa malengo. Sambaza karatasi za mazoezi za kupangia malengo ELEVU na waombe wanafunzi wakamilishe kuzijaza. Malengo ELEVU yako bayana, yanaweza kupimwa, yanafikika, yana umuhimu, na yana muda maalumu. Wanafunzi wanatakiwa kuwa na vipimo bayana vya kupima mafanikio, kupima matokeo, matarajio ya kufikia ambayo ni halisi, sababu nzito kwanini wamechagua kufanya hili jambo, na tarehe bayana ambazo watataka kupima malengo yao.

Kuweka Bajeti

Baada ya hapo, pitisha karatasi ya mazoezi ya bajeti. 'Powerpoint'ya Usimamizi wa Mradi ilihusisha kipande cha kuweka bajeti, lakini hapa wanafunzi watashughulika ili kupanga raslmali muhimu zinazohitajika. Wachochee kufikiria njia za kibunifu kuweza kufanya haya, kama vile kwa kupitia biashara ya mwana familia au rafiki wa karibu. Waombe wakusanye karatasi za mazaezi za kuweka bajeti kwa mwongozaji.

Majadiliano

1. Unahitaji ufadhili wa kiasi gani ili kuhakikisha mradi wako unaanza?
2. Ni vitu gani vitakuwa vimefadhiliwa?
3. Malengo yako ELEVU ni yapi katika mradi wako?
4. Misheni ya mradi wako ni ipi?

KARATASI YA MAZOEZI YA MWANAFUNZI: KUPANGA MALENGO ELEVU

MUDA: DAKIKA 30-40

MAHSUSI

Taja hatua kuanzia 3 ambazo utazichukua kutekeleza mradi wako.

UPIMAJI

Nitapima/kufuatilia mradi wangu kwa kutumia vipimo vifuatavyo:

Nitajua mradi wangu unamafanikio pale ambapo:

KUFIKIA LENGO

Vitu ninavyovihitaji kufikia lengo hili:
Vitu ninavyohitaji kujifunza zaidi kuhusu:
Watu ninaoweza kuongea nao kwa msaada zaidi:

UMUHIMU

Ni kwanini unataka kufanya mradi huu uwe wa mafanikio?

MUDA

Lengo la Kwanza:
Tarehe ya Mwisho: ___ / ___ / ___

Lengo la Pili:
Tarehe ya Mwisho: ___ / ___ / ___

Lengo la Tatu:
Tarehe ya Mwisho: ___ / ___ / ___

KARATASI YA MWANAFUNZI YA MAZOEZI: KUWEKA BAJETI

MUDA: DAKIKA 20-30

UFAFANUZI WA KITU	GHARAMA YA KITU

GHARAMA KAMILI YA MRADI:

KUWASILISHA MAWAZO YAKO

MUDA: DAKIKA 60-75

Kuwa na uwezo wa kuwasilisha mawazo yako na kuelezea hadithi zako ni maarifa ya muhimu sana kwa kiongozi au mwana mabadiliko.

Kuongea mbele Watu
Kuwa msemaji mzuri mbele ya watu kunahusisha utulivu, sauti, maisha, kutazama machoni, vitendo na spidi. Wagawie wanafunzi vitini vya ushauri wa namna ya kuongea mbele za watu ili wavitumie wakati wa kuandika na kufanya mazoezi ya kauli zao. Wanafunzi wataandika na kufanyia mazoezi ya maelezo yao ndani ya makundi yao kabla ya kuyawasilisha baadae mwisho wa siku.

Kuandika Hotuba Yako
Wanafunzi waandae maelezo ya sekunde 120 juu ya wazo lao. Wahusishe jina lao, umri wao, jina la mradi wao, tatizo wanalojaribu kulitatua, suluhisho walilolibuni, na kwanini suluhisho hilo ni la muhimu.

Kuwasilisha Mawazo Yako
Wapatie kila kundi na wazo la kuwasilisha la dakika 3 – 5. Huu ni muda mzuri wa kuwarekodi wakiwasilisha kwa ajili ya matumizi ya maendeleo yao binafsi. Wapatie maoni juu ya mawazo yao na uwasilishaji wao (chanya!) baada ya kumaliza wachochee wanafunzi wengine kutengeneza mazingira ya kuungana mkono kwa kutokuchekana, kuwa watazamaji walio kimya, na kuwapigia makofi wana mabadiliko wenzao pale uwasilishaji unapokamilika.

MAWAZO YA KUFUNGA

MUDA: DAKIKA 60

Kwenye saa la mwisho la programu (baada ya wanafunzi kuwasilisha), endesha majadiliano ya makundi ili wanafunzi wajadiliane ni nini wamejifunza na ni yapi malengo yao ya mbeleni, na namna wanavyoweza kutumia walichojifunza kwa malengo ya mbeleni au miradi mingine.

Mijadala ya mwisho wa Programu:

1. Umejifunza nini wiki hii?
2. Je, unajihisi kuwa mwenye ujasiri zaidi juu ya uwezo wako kuleta mabadiliko?
3. Je, unahisi kwamba malengo ya SDG sasa hivi yanaweza kufikiwa?
4. Je, unajihisi kama kiongozi?
5. Je, utatumiaji maarifa uliyojifunza katika jamii yako?

Uchuguzi wa Baada ya Programu

- Jina (sio lazima)
- Umri:
- Programu ilifanana vipi au ilitofautiana vipi na matarajio yako?
- Je, unajihisi fahari na ulichoweza kukifanya kwa siku mbili tu?
- Umejifunza nini katika kipindi chote cha programu hii?
- Ni kwa namna gani ulichojifunza kina umuhimu kwako au kwa safari yako ya uongozi?
- Unajihisi umepata uwezo wa kuweza kufanya mabadiliko kwenye jamii yako yatakayoonekana?
- Je, unajiona kuwa na uwezo wa kuwa kiongozi?
- Je, malengo yako ya muda mrefu yamebadilika baada ya kipindi cha programu hii?

TUNA IMANI KWAMBA VIJANA WANAUWEZO & WATABADILISHA DUNIA.

AYANA
INTERNATIONAL